

# Lijue Bunge la Tanzania


**Kimetayarishwa na:**

**Ofisi ya Bunge**
**Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano**
**S.L.P. 9133**
**Dar es Salaam**



*Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Job Y. Ndugai (Mb)*

# Lijue Bunge la Tanzania

## YALIYOMO

Historia ya Bunge ........ 1

Muundo wa Bunge ........ 5

Hatua za Utungaji Sheria ........ 13

Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard) ........ 23

Taratibu za Kutembelea Bunge ........ 33

# *Karibu Ulijue Bunge lako*

***Bunge limekuwepo tangu tupate uhuru na kabla ya uhuru kuanzia mwaka 1926. Wabunge nao wameendelea kuwepo kwa vipindi tofauti kwa idadi inayobadilika kila mwaka wakitekeleza wajibu wao muhimu wa kutunga Sheria na kuisimamia Serikali kwa niaba ya Wananchi kwa mujibu wa Katiba ya Nchi.***

***Kitabu hiki kinaelezea historia fupi ya Bunge, Muundo na Majukumu kwa lengo la kukupa fursa ya kulifahamu Bunge na kuelimika kuhusu kazi zake. Tunaamini kitasaidia kutoa mwanga kuhusu kazi za Bunge, Karibuni!***

Dkt Thomas Kashillilah
**Katibu wa Bunge**



# Historia ya Bunge

## *Utangulizi*

Historia ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaanzia mara baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Aidha Bunge la Tanganyika lilianza tarehe 19 Machi 1926 siku ambayo Bunge la Uingereza lilipitisha Sheria iliyoitwa "The Tanganyika (Legislative Council) Order in Council, 1926" Kipindi hicho likijulikana kama Baraza la Kutunga Sheria la Tanganyika.

Tanganyika wakati huo ilikuwa chini ya Utawala wa Ui ngereza ambayo ilikuwa imepewa mamlaka na Umoja wa Mataifa (League of Nations) kuisimamia Tanganyika hadi ipate Uhuru wake. Sheria hiyo ambayo ilitaka kuanzishwa Baraza la Kutunga Sheria, ilichapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 18 Juni 1926. Baraza hilo liliitwa "The Legislative Council of Tanganyika Territory" na kujulikana zaidi kwa kifupi kama "LEGCO". Baraza hili lilizinduliwa tarehe 7 Desemba 1926 mjini Dar es salaam chini ya Uenyekiti wa Gavana Sir Donald Cameron likiwa na Wajumbe 20 wote wakiwa wameteuliwa na Gavana. Sheria zote zilizokuwa zikitungwa na Baraza ahili zilikuwa zinapelekwa Uingereza kwa ajili ua kupata Idhini ya Mkuu wa Nchi kabla ya kuanza kutumika.

## *Mabadiliko Mbali Mbali*

Mabadiliko makubwa ya kwanza kufanyika katika Baraza la Kutunga Sheria yalikuwa mwaka 1953 wakati Gavana alipoondolewa kuongoza Baraza na nafasi yake kuchukuliwa na Spika Brigedia Willam Erick Halstead Sculpham, aliyeapishwa tarehe 1 Novemba 1953 kuwa Spika wa kwanza wa Baraza hilo. Aidha, utaratibu ukibadilika kwa Sheria zilizotungwa na Baraza kuanza kuidhinishwa na Gavana kwa niaba ya Mfalme/Malkia wa Uingereza

Mabadiliko ya pili makubwa yalikuwa mwaka 1958 ambapo kwa mara ya kwanza Baraza lilipata Wajumbe wa kuchaguliwa na watu. Katika uchaguzi uliofanyika mwaka huo, vyama vitatu vya Siasa ambavo ni Tanganyika African National Union (TANU), United Tanganyika Party (UTP) na African National Congress (ANC) vilishiriki. Chama cha TANU pekee kilishinda katika baadhi ya majimbo na hivyo kukifanya chama hicho kuwa cha kwanza kushiriki kwenye LEGCO.

Mabadiliko makubwa ya tatu yalitokea mwaka 1960 kwenye uchaguzi wa pili ambao ulikuwa ni sehemu ya maandalizi ya Uhuru wa Tanganyika ambapo wajumbe wote walichaguliwa. Aidha, jina la chombo hiki lilibadilika kutoka kuwa Baraza la Kutunga Sheria na kuwa Bunge (National Assembly) mwaka 1961. Lengo lilikuwa ni kuandaa mfumo ili baada ya uhuru Rais wa Tanganyika awe na mamlaka kikatiba ya kutoa idhini kwa sheria zitakazotungwa na Bunge

Baada ya Uhuru wa Tanganyika mwaka 1961, pamekuwa na mabadiliko makubwa mengine matatu yakiwa ni: Bunge kuwa na sura ya Muungano mwaka 1964, Bunge kuwa la Chama Kimoja mwaka 1965 na kurejeshwa kwa mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa nchini mwaka 1992 ambao ulilifanya Bunge kuwa la vyama vingi kuanzia mwaka 1995. Aidha, katika kipindi chote kilichopita yamekuwepo mabadiliko madogo madogo ya idadi na aina za Wabunge.



*Rais wa Awamu ya Kwanza wa Tanzania Mwalimu Julius K. Nyerere akihutubia Bunge la Tanzania katika Ukumbi wa karimjee Jijini Dar es Salaam mwaka 1968*

### Kumbi zilizowahi kutumika na Bunge

Baraza la Kutunga sheria liliwahi kufanya vikao vyake awali kwenye ukumbi wa Anatouglou na baadaye kuhamia jengo ambalo siku hizi linaitwa Freemason Hall. Baada ya hapo Bunge likawa likikutana katika Ukumbi wa Karimjee mjini Dar es salaam. Kutokana na Azimio la Serikali la mwaka 1971 la kuifanya Dodoma kuwa Makao Makuu ya Chama na Serikali tangu mwaka 1974, Mikutano midogo ya Bunge isipokuwa Mikutano Maalum ilianza kufanyika kwenye ukumbi wa CCM Dodoma huku Mkutano wa Bajeti ukiendelea kufanyika katika Ukumbi wa Karimjee Dar es salaam. Utaratibu



*Sehemu ya Ndani ya Ukumbi wa Sasa wa Bunge la Jamhuri Uliopo Dodoma*

huu uliendelea hadi mwishoni mwa miaka ya tisini ndipo Bunge lilipoanza kufanya mikutano yake yote Dodoma kwenye ukumbi wa Pius Msekwa na baadaye kwenye ukumbi mpya wa Bunge uliopo sasa

### Ukumbi wa Sasa wa Bunge

Ukumbi wa Bunge unaotumika hivi sasa uko Dodoma. Ulizinduliwa rasmi na kuanza kutumika mwaka 2006. Katikati ya Jengo la Bunge ndipo ulipo ukumbi unaotumika kwa shughuli za vikao vya Bunge. Pembeni kuna maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili makundi mbalimbli ya watu kama ifuatavyo:

1. Majukwaa mawili kwa ajili ya wananchi (Public Galleries) wanaopata fursa ya kulitembelea Bunge na kuhudhuria Vikao vya Bunge. Maeneo haya yana uwezo wa kuchukua wageni 84 kila moja.
2. Jukwaa maalum kwa wageni wa Spika (Speaker's Gallery). Eneo hili ni kwa ajali ya wageni mashuhuri na wageni wengine wa Spika na lina uwezo wa kuchukua wageni 40 waliokaa




*Ukumbi wa Karimjee Dar es Salaam uliwahi kutumiwa na Bunge la Tanganyika*

3. Majukwaa matatu kwa ajili ya Maafisa wa Serikali kutoka Wizara mbalimbali (Government Official Gallleries ) wanaokuja Bungeni. Maeneo haya yana uwezo wa kuchukua watu 25 kila moja.

4. Jukwaa moja kwa ajili ya Waandishi wa Habari (Press Gallery) ambao huripoti habari za Bunge wakati mikutano ya Bunge. Eneo hili lina uwezo wa kuchukua watu 25.

*******

# *Muundo na Majukumu ya Bunge*

Ibara ya 62 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ndiyo inayoweka uwepo wa Bunge la Tanzania. Ibara ya 63 na 64 za Katiba hiyo zinalipa Bunge mamlaka na madaraka lililonalo. Hivyo basi, Muundo wa Bunge pamoja na majukumu yake vimewekwa bayana katika Katiba ya nchi.

## *Muundo*

Muundo wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania umeelezwa katika Ibara ya 66 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kama ilivyorekebishwa chini ya mabadiliko ya 5 na 14. Kuna aina kuu 6 za Wabunge kama ifuatavyo:

Muundo wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania umeelezwa katika Ibara ya 66 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kama ilivyorekebishwa chini ya mabadiliko ya 5 na 14. Kuna aina kuu 6 za Wabunge kama ifuatavyo:

- Wabunge waliochaguliwa moja kwa moja kuwakilisha Majimbo ya uchaguzi. Idadi yao kwa sasa ni 264. (Tanzania Bara 214 na Tanzania Visiwani – Zanzibar 50)
- Wabunge kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Idadi yao ni Wabunge watano.
- Wabunge wa Viti Maalum Wanawake. Idadi yao ni 113 ikiwa ni asilimia 40 ya jumla ya Wabunge wote.
- Wabunge wasiozidi (10) wa kuteuliwa na Rais.
- Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye huingia Bungeni kwa nafasi yake.
- Spika wa Bunge iwapo hatokani na Wabunge waliotajwa hapo juu.

Jumla ya Wabunge wote Kikatiba kwa sasa ni 393. (idadi hii inaweza kubadilika kutokana na hali ya siasa na mahitaji ya nyakati zijazo)

## Majukumu

Majukumu ya Bunge yametamkwa katika Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Nchi, kwa maneno yafuatayo:

> *"Sehemu ya pili ya Bunge itakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano, ambacho kitakuwa na madaraka, kwa niaba ya Wananchi, ya kusimamia na kuishauri Serikali ya Muungano pamoja na mvyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake "*

Hivyo basi Bunge ni Chombo cha Uwakilishi wa Wananchi. Kwa madhumuni ya utekelezaji wa madaraka yake Bunge linaweza:-

- Kumuuliza Waziri yeyote swali lolote kuhusu mambo ya Umma.
- Kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila mwaka wa Bajeti.
- Kujadili na kuridhia Mpango wowote wa muda mrefu au muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutunga Sheria ya kusimamia utekelezaji wa Mpango huo.
- Kutunga Sheria pale ambapo utekelezaji unahitaji kuwapo Sheria.
- Kujadili na kuridhia Mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ambayo kwa masharti yake inahitaji kulidhiwa

## Uendeshaji Wa Shughuli Za Bunge

Ibara ya 96 ya katiba inalipa Bunge uwezo wa kuunda kamati za Bunge za namna mbali mbali kadri litakavyoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora wa madaraka yake. Ibara ya 89 inalipa Bunge mamlaka ya kutunga Kanuni za Kudumu kwa ajili ya kuweka utaratibu wa kutekeleza shughuli zake.



*Moja ya Kamati za kudumu ya Bunge ikitekeleza majukumu yake wakati wa vikao vya kamati katika Ofisi Ndogo za Bunge Jijini Dar es Salaama*

Kanuni ya 118 ikisomwa pamoja na Nyongeza ya Nane ya Kanuni za kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 inataja Kamati za kudumu za Bunge zilizoanzishwa chini ya Ibara ya 96 ya Katiba

## *Aina Za Kamati*

Kimsingi kuna aina mbali mbali za kamati za Bunge: Kamati za kudumu (Kan: 118), Kamati Teule (Kan.120), Kamati ya Matumizi (Kan. 100), Kamati ya Bunge Zima (Kan.3 na 88) Kamati ya Mipango (Kan.3 na 94), Kamati za vyama Vya Siasa (Kan.112). Kwa madhumuni ya kuongeza uelewa, aina za kamati za kudumu za Bunge na Kamati Teule zinaelezwa kwa kina.

### Kamati za Kudumu za Bunge

a) Kamati za kudumu za Bunge zisizo za Kisekta

**Kuna kamati tatu (3) za kudumu za Bunge ambazo si za kisekta. Kamati hizo ni:**

i) kamati ya Uongozi;

ii) Kamati ya Kanuni za Bunge; na

iii) Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

### b) Kamati za kudumu za Bunge za Kisekta

Kamati tisa (9) za kudumu za Bunge ni Kamati za Kisekta. Kamati hizo ni:-

i) Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira

ii ) Kamati ya Katiba na Sheria

iii) Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama;

iv) Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa;

v) Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii;

vi) Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii;

vii) Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji;

viii) Kamati ya Miundombinu;

ix) Kamati ya Nishati na Madini.

**c) Kamati za kudumu za Sekta Mtambuka**

Kuna Kamati nne (4) za Sekta Mtambuka. Kamati hizo ni:-

i) Kamati ya Bajeti

ii) Kamati ya Masuala ya UKIMWI;

iii) Kamati ya Sheria Ndogo;

iv) Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma.

**d) Kamati za kudumu za Bunge zinazosimamia matumizi ya fedha za Umma**

Zipo Kamati mbili (2) za kudumu za Bunge zinazosimamia matumizi ya fedha Umma. Kamati hizo ni:-

i) Kamati ya Hesabu za Serikali

ii) Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC)

## *Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati za Kudumu Za Bunge*

Kama ilivyoelezwa hapo mwanzo, Kamati za Bunge ni vyombo muhimu vya kuliwezesha Bunge kufanya shughuli zake. Ni kwa msingi huo, Sehemu kubwa ya shughuli za Bunge hutekelezwa kwenye Kamati za Bunge na Taarifa ya Kamati hizo huwasilishwa Bungeni ili uamuzi wa kibunge ufanyike. Shughuli hizo ni Pamoja na:-




*Wajumbe wa Mojawapo ya Kamati za kudumu za Bunge wakiwa katika ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo*

i) Kushughulikia Bajeti za Wizara zinazosimamiwa na Kamati za Kisekta

ii) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba ya Kimataifa inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara zinazozisimamia na Kamati za kisekta

iii) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila Mwaka za Wizara

iv) Kufuatilia Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara

v) Kuimarisha Ushirikiano kati ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mabunge mengine;

vi) Kufuatilia Mwenendo wa hali ya Mtangamano wa Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za kusini mwa Afrika

vii) Kupitia na kujadili taarifa za hali ya Ulinzi na Usalama wa mipaka ya nchi na Usalama wa Raia na mali zao

viii) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Serikali kuhusu UKIMWI na Udhibiti wa Madawa ya Kulevya;

ix) Kujadili na kutoa mapendekezo na ushauri kuhusu hatua za kudhibiti madawa ya kulevya;

x) Kuchambua na kubaini iwapo utekelezaji miradi ya uwekezaji wa Umma una ufanisi na kuwa umezingatia taratibu na Sheria na miongozo mujarabu ya biashara; na

xi) Kuchambua na kujadili Taarifa ya Mwaka ya Msajili wa Hazina na Mashirika ya Umma na kampuni ambazo Serikali ina Hisa

xii) Kushughulikia Maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za Umma

*******

# Hatua za Utungaji Sheria

Katika mgawanyo wa madaraka nchini, Ibara ya 4 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imelipa Bunge mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Umma nchini. Ibara ya 64 ya Katiba inabainisha jukumu la kutunga sheria juu ya mambo yote yahusuyo Tanzania Bara chini ya Bunge la Jamhuri ya Muungano.

Ili kutekeleza majukumu yake likiwemo jukumu la kutunga Sheria, Ibara ya 89 (1) ya Katiba, imetoa mamlaka kwa Bunge kutunga Kanuni za Kudumu kwa ajili ya kuweka utaratibu wa kutekeleza shughuli zake. Kwa mujibu wa mamlaka hayo, Sehemu ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 imeweka masharti ya jumla kuhusu utungaji wa Sheria kuanzia utangazaji wa Miswada ya Sheria hadi muswada uliopitishwa na Bunge kupata ridhaa ya Rais na hifadhi ya sheria.

## *Aina za Miswada*

Utaratibu wa kutunga sheria unahusisha kuwepo kwa Muswada ya Sheria kabla ya Sheria yenyewe. Muswada wa Sheria ni Hati rasmi ya sheria inayokusudiwa kutungwa ambayo huwasilishwa Bungeni, kujadiliwa na kisha kupigiwa kura. Zipo aina kuu mbili za Miswada ya Sheria ambazo ni: Kwanza, Miswada ya Serikali na Pili Miswada Binafsi. Kanuni ya 81 inataja Miswada Binafsi ya namna mbili; Muswada wa Kamati ya kudumu ya Bunge na Muswada wa Mbunge binafsi.

## *Hatua Muhimu Za Utungaji Sheria*

Kabla ya kuwa Sheria, Muswada hupitia hatua kadhaa ikiwa ni pamoja na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali, Kusomwa Bungeni na kisha kupata ridhaa ya Rais. Kanuni ya 80 (1) ya Kanuni za Bunge imeweka sharti la Muswada kutangazwa

kwenye Gazeti maalumu la Serikali katika matoleo angalau mawili. Hatua za uchapishaji baina ya matoleo hayo hazitakiwi kupungua siku saba.

Katika Tangazo la kwanza la Muswada wa Sheria kutoka Serikalini Muswada mzima utaoneshwa ikiwa ni pamoja na maelezo kuhusu madhumuni ya Muswada husika yaliyotiwa saini na Waziri au Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Iwapo ni Muswada binafsi wa Kamati au wa Mbunge, saini itawekwa na Mwenyekiti wa Kamati au Mbunge anayehusika.

Tangazo la Muswada wa Serikali kwa mara ya pili litafanyika kwa kutoa taarifa katika Gazeti la Serikali kwa kutaja jina la Muswada, Nambari na tarehe ya Gazeti ambapo Muswada huo ulitangazwa mara ya kwanza.

## *Muswada kusomwa na Kujadiliwa Bungeni*

Kabla ya Muswada Kusomwa Bungeni kwa mara ya kwanza, Tangazo la kwanza la Muswada wa Sheria zilizotolewa litamfikia Katibu wa Bunge katika muda usiopungua siku 21 kabla ya Muswada huo kusomwa Bungeni kwa mara ya kwanza.

Muswada wa Sheria uliomfika Katibu wa Bunge mara baada ya kutangazwa unaweza kuwekwa kwenye Orodha ya Shughuli za Bunge kwa mara ya kwanza. Katika hatua hii Katibu atasoma jina refu la Muswada husika bila hoja yoyote kutolewa kwa ajili ya Muswada huo. Unaposomwa Muswada kwa mara ya kwanza hakuna mjadala wowote kuhusu muswada huo.

Baada ya Muswada Kusomwa mara ya Kwanza Spika anaupeleka kwenye Kamati inayohusika ambayo itaanza kuujadili mapema iwezekanavyo. Kamati hiyo inatakiwa kutoa matangazo au itatoa barua ya mwaliko kwa lengo la kuwakaribisha watu mbali mbali kutoa maoni yao kwa Kamati inayohusika na kuisaidia kufanya uchambuzi.



*Waziri Mkuu ambaye ni kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni akijibu maswali ya papo kwa papo Bungeni wakati wa kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu*

## *Uwezo wa Kamati Kufanya Marekebisho Katika Muswada*

Kamati inayohusika na Muswada itakuwa na uwezo wa kufanya marekebisho katika Muswada wa Sheria. Masharti ya kutumia uwezo huo yameelezwa katika kanuni ya 84 (3) ambapo inatoa masharti kwa kamati kufanya marekebisho kwa kumshauri mtoa hoja. Iwapo ni Muswada wa Kamati ya kudumu ya Bunge au ni Muswada wa Mbunge Binafsi, Serikali nayo imepewa uwezo wa kufanya marekebisho ya Muswada huo kwa kumshauri Mbunge au Kamati inayotoa hoja.

Ikiwa Muswada huo utakuwa umefanyiwa marekebisho utapelekwa tena Kwenye Kamati inayohusika. Lengo ni kuiwezesha Kamati hiyo kuzingatia mabadiliko yaliyowekwa. Baada ya Kamati kukamilisha kazi itamwarifu Spika kuwa imekamilisha kazi ili kwenda kwenye hatua inayofuata.

## *Muswada Kusomwa Mara ya Pili*

Katika hatua hii, mtoa hoja atatoa hoja kwamba Muswada usomwe Mara ya Pili na atauwasilisha na kutoa maelezo ya ufafanuzi. Kanuni ya 86 (5)inataka baada ya mtoa hoja kutoa maelezo ya ufafanuzi Mwenyekiti wa Kamati iliyopelekewa Muswada wa Sheria au mjumbe mwingine yeyote aliyeteuliwa kwa madhumuni hayo atatoa maoni ya Kamati kuhusu Muswada huo.

Kama ni Muswada wa Serikali, Msemaji wa Kambi ya Upinzani atafuata baada ya Mwenyekiti na atatoa maoni ya Kambi yake kuhusu Muswada huo. Iwapo ni Muswada Binafsi, Msemaji wa Serikali atatoa maoni yake baada ya Mwenyekiti. Hatua itakayofuata ni mjadala kuhusu Muswada. Kanuni ya 86 (7) inataka mjadala huo uhusu ubora na misingi ya Muswada huo tu

## Mabadiliko Katika Muswada

Muswada na mapendekezo kuhusu sheria inayokusudiwa na Utungaji wa sheria ni jukumu la Bunge lenyewe. Wakati wa mjadala, kanuni ya 86 (9-11) imetoa fursa na masharti ya kufanya mabadiliko katika Muswada kwenye hatua ya mjadala baada ya kusomwa Mara ya Pili. Mbunge yeyote au Waziri anaruhusiwa kumshauri mtoa hoja afanye mabadiliko katika Muswada, ama mabadiliko ya jumla au yale atakayoyataja Mbunge.
Ikitokea mtoa hoja anataka kufanya mabadiliko kwenye Muswada kutokana na ushauri uliotolewa au kwasababu nyingine yoyote, atapaswa kumjulisha Mwandishi Mkuu wa Sheria kama ni Muswada wa Serikali. Ikiwa ni Muswada Binafsi mtoa hoja atamjulisha Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria. Taarifa hiyo inalenga kuwezesha kutayarishwa kwa mabadiliko hayo na kukabidhiwa kwa Katibu wa Bunge. Kuna namna mbili za kuweka marekebisho ambazo ni:-

i) Kuuchapisha upya Muswada wa Sheria ukiwa na marekebisho au mabadiliko yanayokusudiwa kufanyika;
ii) Kuwa na Jedwali la Marekebisho au Mabadiliko yanayokusudiwa kufanyika.

Mabadiliko mengine mbali na yale ya mtoa hoja yanaweza kufanywa na Kamati ya Bunge au Mbunge kwa kuwasilisha mabadiliko yanayokusudiwa kufanywa katika muswada huo. Namna ya kuwasilishwa kwa mabadiliko hayo imeelezwa katika Kanuni ya 86 (11) ambapo mtoa hoja anatakiwa kuwasilisha kwa maandishi kwa Katibu wa Bunge akionyesha bayana mabadiliko yanayokusudiwa kufanyika katika Ibara inayohusika, wakati wa Kamati ya Bunge Zima.

## ***Kurejeshwa Muswada Kwenye Kamati***

Kanuni ya 87 (1) inaruhusu mtoa hoja kuomba Muswada uliokwishasomwa Mara ya Pili na haukuwa na mabadiliko urejeshwe kwenye Kamati. Ombi hili linaruhusiwa iwapo kuna jambo au suala jipya lilitokea ambalo linahitaji kushughulikiwa. Ruhusa hii inatolewa wakati wowote kabla ya Muswada kusomwa Mara ya Tatu.

Kwa mantiki hiyo, Kamati iliyopelekewa Muswada itakuwa na mamlaka ya kufanya mabadiliko katika Muswada uliopelekwa kwake kufuatia ombi la kuurejesha Muswada huo kwenye Kamati. Fasili ya 4 ya Kanuni iliyotajwa hapo juu inaeleza namna mbili zinazoweza kutumiwa na Kamati kuweza kufanya mabadiliko. Namna hizo ni:

a) Kumshauri Waziri, Kamati au Mbunge anayehusika na Muswada kufanya mabadiliko katika Muswada huo.
b) Kupitisha Azimio la Kutoa Bungeni Taarifa maalumu kuhusu Muswada huo.

Baada ya Kamati kumaliza kuujadili Muswada kwa Mara ya Pili, Muswada huo utapelekwa katika Kamati ya Bunge Zima. Endapo Kamati iliyoujadili Muswada Mara ya Pili italazimika kuwasilisha Bungeni taarifa maalumu juu ya muswada huo, Mwenyekiti wa Kamati atamjulisha Spika na taarifa hiyo itatolewa na Mwenyekiti au mjumbe mwingine wa Kamati kwa niaba ya Mwenyekiti kabla ya Muswada huo kuwasilishwa kwenye kamati ya Bunge Zima.

## ***Muswada Kwenye Kamati ya Bunge Zima***

Baada ya Bunge kuujadili Muswada, hukaa kamati
ya Bunge Zima. Katika hatua hii, kanuni ya 88 (10) inaelekeza Kamati ya Bunge Zima kujadili na kupitisha au kufanya

Mabadiliko au kuupitisha Muswada wa Sheria, Ibara moja baada ya nyingine. Utaratibu wa Muswada kupitishwa au kutopitishwa hutekelezwa kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge Zima kuihoji Kamati hii kuamua katika sehemu moja moja zenye Ibara kadhaa au Ibara zote zilizomo katika sehemu moja ya Muswada. Namna ya kuhoji itategemea Mwenyekiti atakavyoona inafaa. Kamati ya Bunge Zima itakapokamilisha kazi ya Muswada wa Sheria, Bunge litarejea na mtoa hoja atatoa Taarifa kuhusu namna Kamati ya Bunge Zima ilivyopitisha Muswada huo na kutoa hoja kuliomba Bunge kwamba liikubali kuupitisha Muswada wa Sheria atakaoutaja.
Iwapo katika hatua hii mtoa hoja atataka kuuondoa Muswada wa Sheria, Kanuni ya 90 imeweka masharti ya kufanya hivyo ambapo imeeleza kuwa anaweza kufanya hivyo wakati wowote lakini si kabla ya Bunge kuhojiwa na kutoa uamuzi wake. Sharti muhimu ni mtoa hoja kutoa taarifa kwa Spika kabla ya kuuondoa Muswada wa Sheria.

## *Muswada Kusomwa Mara ya Tatu*


Bunge linaporejea, Mtoa hoja hutoa Taarifa kwamba kamati ya Bunge Zima imemaliza kuupitia Muswada ndipo Bunge huhojiwa ili kufanaya uamuzi. Baada ya Bunge kuamua, Muswada wa Sheria utasomwa Mara ya Tatu ambapo Katibu atasoma jina fupi la Muswada. Kanuni ya 91 ya Kanuni za kudumu za Bunge inaeleza kuwa baada ya Muswada kusomwa Mara ya Tatu utahesabika kuwa umepitishwa na Bunge.

## *Muswada wa Dharura*

Serikali inaweza kuwasilisha muswada kwa dharura ili usomwe na kupitia kwenye hatua zote katika Mkutano mmoja. Ili hilo liweze kufanyika, ni lazima Muswada unaowasilishwa uambatane na Hati ya dharura iliyosainiwa na Rais. Muswada huo utawasilishwa kwanza kwenye kamati ya Uongozi (Kan. 80 (3) na (4)).



*Wabunge wakiendelea na majadiliano Bungeni katika moja ya majukumu yao ya Utungaji wa Sheria*



THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

No. 36 of 1972

I ASSENT,

President

23rd November, 1972

**An Act to apply a further sum of fifty-two million four hundred ninety-six thousand two hundred seventy-nine shillings out of the Consolidated Fund to the Service of the year ending on the thirtieth day of June, one thousand nine hundred and seventy-three and to appropriate the supply granted**

[24th November, 1972]

Enacted by the Parliament of the United Republic of Tanzania.

1.—(1) This Act may be cited as the Supplementary Appropriation (No. 1 for the Financial Year 1972/73) (No. 5) Act, 1972 and shall be read as one with the Appropriation Act, 1972. *Short title and interpretation*


(2) The expressions used in this Act shall have the meanings respectively ascribed thereto in the Exchequer and Audit Ordinance. *Cap. 439*

2. The Treasury may issue out of the Consolidated Fund and apply towards the supply granted for the service of the year ending on the thirtieth day of June, 1973, the sum of fifty-two million four hundred ninety-six thousand two hundred seventy-nine shillings. *Issue of Shs. 52,496,279 out of the Consolidated Fund*

3. The sum granted by section 2 shall be appropriated to the purposes and in the amounts specified in the second and fifth columns of the Schedule to this Act. *Appropriation of moneys voted*

4.—(1) The Minister may at any time or times not later than the thirtieth day of June, 1973, borrow within or outside Tanzania or partly within and partly outside Tanzania any sum or sums not exceeding in the whole fifty-two million four hundred ninety-six thousand two hundred seventy-nine shillings by way of loan, advance, the issue of bills or bank overdraft and on such terms and conditions as the Minister may deem expedient, and may charge any such loan or advance on any of the assets of the United Republic (including securities forming part of the Consolidated Fund). *Powers of the Minister to borrow*

1



THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

No. 12 of 1987

I ASSENT,

President

**An Act to amend the Economic and Organized Crime Control Act, 1984**

[..............................]

Enacted by the Parliament of the United Republic of Tanzania.

1. This Act may be cited as the Economic and Organized Crime Control (Amendment) Act, 1987, and shall be read as one with the Economic and Organized Crime Control Act, 1984, in this Act referred to as "the principal Act". *Short title and construction* *Acts, 1984 No. 13*


2. Section 4 of the principal Act is hereby amended by deleting sub-section (2) and the character "(1)" occuring in the first line of that section. *Amendment of section 4*

3. Section 5 of the principal Act is hereby amended by deleting sub-sections (4) and (5) and substituting for them, respectively, the following: *Amendment of section 5*

"(4) The High Court shall select and summon two persons from among the list submitted by the Regional Judicial Board to be lay members for the purposes of each session or, if one case only is to be heard, for the purposes of the case concerned."

"(5) Where a lay member becomes unable to sit on the Court after proceedings in any case have commenced, and such inability is expected to last unduly long, the proceedings may continue until the conclusion of that case or, if at a session, of all the other cases, notwithstanding the absence of that member."

1



THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

No. 20 of 1999

I ASSENT,

Benjamin W. Mkapa

President

22nd December, 1999.

**An Act to apply a sum of two thousand seven hundred and sixty-seven million one hundred ninety-three thousand, nine hundred thirty-four shillings out of the Consolidated Fund to the Service of the year ending on the thirtieth day of June, 1995, and to appropriate the supply granted.**


[..............................]

Enacted by the Parliament of the United Republic of Tanzania

1.-(1) This Act may be cited as the Supplementary Appropriation (For Financial Year 1994/95) (No. 3) Act, 1999, and shall be read as one with the Appropriation Act, 1994. *Short title and interpretation No. 14*

(2) The Expressions used in this Act Shall each have the meaning ascribed to it in the Exchequer and audit Ordinance *Cap. 439*

1



4 No. 2 *Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3)* 2010

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

NO. 2 OF 2010

I ASSENT,

*President*

17th March, 2010

**An Act to amend certain written laws.**

Enacted by Parliament of the United Republic of Tanzania.

PART I

Preliminary Provisions

*Short title* 1. This Act may be cited as the Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Act, 2010.

*Amendment of certain written laws* 2. The Written Laws specified in various Parts of this Act are amended in a manner provided for in their respective Parts.

*Mwonekano wa baadhi ya sheria zikiwa zimetiwa saini na Waheshimiwa Marais wa Awamu zote nne baada ya kupitishwa na Bunge*

## *Ridhaa ya Rais na Hifadhi ya Sheria*

Muswada kama ulivyopitishwa na Bunge hutayarishwa chini ya uangalizi na usimamizi wa Katibu wa Bunge kwa kuingiza mabadiliko yote yaliyofanyika. Katibu huwasilisha nakala moja ya Muswada huo kwa Rais mapema ili Rais atoe kibali chake kwa mujibu wa Ibara ya 97 (1) ya Katiba na pia nakala moja kwa Spika kwa taarifa. Hifadhi ya nakala halisi iliyopata kibali cha Rais ni dhamana aliyokabidhiwa katibu wa Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 92 (2) ya Kanuni za kudumu za Bunge.

*******

# Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard)

## *Historia*

Neno Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard) limetokana na familia ya wachapaji ya Luke Hansard ya nchini Uingereza ambayo ilikuwa inajihusisha na uchapaji wa taarifa mbalimbali ikiwemo Majadiliano ya Bunge. Mwaka 1752 mpaka 1909 Bunge Dogo (Makabwela) la Uingereza (House of Commons) ndilo ambalo lilianza kutoa Taarifa Rasmi za Majadiliano ya Bunge na kufuatiwa na Bunge Kubwa (Mabwanyenye) (House of Lords) mwaka 1917 na Mabunge yote mawili yaliamua kutumia jina la Hansard kwa Majadiliano hayo ya Bunge ili kuenzi kazi kubwa iliyofanywa na familia hii. Baada ya hapo nchi zilizotawaliwa na Uingereza (Commonwealth Countries) Tanzania ikiwa mojawapo ziliamua kufuata mfumo huo wa utunzaji wa Majadiliano ya Bunge na kuendelea kuyaita majadiliano hayo Hansard.

Hapa nchini, historia ya Hansard ilianzia mwaka 1926 (wakati huo ikijulikana kama Tanganyika) katika Bunge la kwanza lililokuwa chini ya Serikali ya Utawala wa Kikoloni wa Kiingereza. Jina hilo limeendelea kutumika mpaka leo.

Kwa kifupi neno Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard) ni Taarifa Rasmi za Majadiliano yote ya Mikutano ya Bunge au Vikao vya Kamati ambapo inahusisha uwekaji wa kumbukumbu wa neno kwa neno (verbatim) wa kila kinachosemwa, kufanyika au kutokea ndani ya Ukumbi wa Bunge au Kamati. Aidha, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limekwenda hatua moja mbele zaidi kwa kuruhusu uchangiaji kwa njia ya maandishi kuwa sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard). Hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 60(14) na (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge (Toleo la Januari, 2016). Hii ilitokana na kuona muda wa kuchangia wa dakika kumi na tano (15) wanaopewa Waheshimiwa Wabunge hautoshi wote kuweza kupata nafasi ya kuchangia na pengine ingelazimu Bunge kukaa kwa muda mrefu zaidi.

Katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard) hutekelezwa kwa mujibu wa Kanuni ya 148(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge (Toleo la Januari, 2016). Kanuni hizi zinaelekeza Hansard kuandikwa katika lugha iliyotumiwa na msemaji (ikumbukwe kuwa lugha rasmi Bungeni ni Kiswahili na Kiingereza) na yakiwa ni maneno halisi aliyoyatamka. Pia atapewa nakala ya alichozungumza ili asahihishe makosa ya kiuchapaji na sio kubadili maana halisi ya maneno aliyoyatamka Bungeni.

Umuhimu wa kuwa na Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard) ni kutumika kama kumbukumbu ambazo zinaweza zikarejewa na Mbunge, Serikali au mtu yeyote wakati wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa jambo fulani lililozungumzwa Bungeni, kutumika kama ushahidi, kutumika kwa ajili ya tafiti mbalimbali na kadhalika.

## *Majukumu ya Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge*

a) Sehemu ya Taarifa Rasmi

1. Kurekodi Majadiliano ya Vikao vya Kamati na Mikutano ya Bunge
2. Kuchapa (transcribing) Majadiliano ya Vikao vya Kamati na Mikutano ya Bunge
3. Kusoma na kuhakiki (proof reading)
4. Kuandaa na kusambaza rasimu (draft) ya Majadiliano ya Vikao vya Kamati na Mikutano ya Bunge.

b) Sehemu ya Uhariri

1. Kuhariri neno kwa neno Majadiliano ya Vikao vya Kamati na Mikutano ya Bunge
2. Kupanga Kurasa za Majadiliano ya Vikao vya Kamati na Mikutano ya Bunge
3. Kupeleka katika Tovuti ya Bunge Majadiliano ya Vikao vya Mikutano ya Bunge

C) Sehemu Ya Uchapaji

1. Kuandaa na kuvifanyia usafi vifaa vinavyotumika katika uchapaji
2. Kushiriki katika utengenezaji wa nyaraka mbalimbali
3. Kuandaa kazi kwa ajili ya uchapaji
4. Kupiga chapa nyaraka mbalimbali
5. Ukarabati mdogo wa mashine
6. Kusanifu na kusadifu nyaraka mbalimbali
7. Kuendesha mashine za uchapaji
8. Kukarabati nyaraka mbalimbali
9. Kupanga nyaraka kulingana na ukubwa na aina yanyaraka kabla ya kuchapa
10. Kufunga machapisho mbalimbali (binding) kulingana na uhitaji wa mteja
11. Kuratibu ubora wa kazi (Quality control).

*******

# *Taratibu za Kutembelea Bunge*

Bunge ni Chombo cha uwakilishi wa Wananchi kama Ibara ya 62 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inavyotumika:

> *"Kutakuwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano ambalo litakuwa na sehemu mbili, yaani Rais na Wabunge. Rais kama sehemu moja ya Bunge atatekelezza yote aliyokabidhiwa na katiba hii. Sehemu ya pili yya Bunge itakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka, kwa niaba ya wananchi, kuisimamia na kuishauri serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii"*

Kimsingi, Bunge ni chombo cha uwakilishi wa wananchi. Kwa kuwa haiwezekani wananchi wote kukusanyika mahali pamoja na kufanya maamuzi muhimu katika uendeshaji wan chi, uwakilishi hauna budi kuwepo. Hii inamaanisha kwamba Wabunge wanapokuwa Bungeni hutekeleza majukumu yao kwa niaba ya wananchi.

Ofisi ya Bunge, kwa kutambua hilo imeweka utaratibu ambapo jamii huruhusiwa kushuhudia namna ambavyo wawakilishi wa wananchi wanavyotekeleza majukumu yao.

## *Wageni Bungeni*

Bunge hufanya mikutano yake mara nne kwa mwaka Mjini Dodoma. Wakati wa mikutano hiyo, watu mbalimbali huruhusiwa kutembelea Bunge na kujionea jinsi linavyoendesha shughuli zake. Kanuni ya 136 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inaeleza ifuatavyo:

> *"Wageni wanaweza kuruhusiwa kuingia kwenye Ukumbi wa Mikutano ya Bunge katika sehemu yoyote ya Ukumbi huo ambayo itatengwa kwa ajili yao"*

Utaratibu wa kutembelea Bunge upo wazi ambapo Watu binafsi, vikundi, Watumishi wa Taasisi za Serikali, Mabalozi wanaowakilisha mataifa yao nchini, Mashirika ya Kidini, Asasi za Kiraia, Taasisi za Kijamii, Wanafunzi (Shule za Awali, Msingi, Sekondari na Vyuo vya Elimu ya Juu) na Wageni kutoka Mabunge nje ya Tanzania au Taasisi za Kimataifa hutumia fursa iliyopo kutembelea Bunge na kuona jinsi linavyoendesha shughuli zake.

Utaratibu mzuri unaopaswa kufuatwa na wanaotaka kutembelea Bunge ni kuandika barua ya maombi ya kutembelea Bunge. Barua hiyo ni vyema ikaeleza tarehe inayokusudiwa, idadi na madhumuni ya kutembelea Bunge na kutumwa kwa anwani ifuatayo:

Katibu wa Bunge
S.L.P 941
DODOMA

Au

Katibu wa Bunge
S.L.P 9133
DAR ES SALAAM

Ofisi ya Bunge hujibu barua zote za maombi ya kutembelea Bunge. Maombi yote yatakayozingatia utaratibu hukubaliwa kama yalivyo, isipokuwa tu kama maombi mengi yamegongana tarehe na idadi ya watu ni kubwa kuzidi uwezo wa maeneo maalumu yaliyotengwa kwa ajili ya wageni. Ikitokea hivyo, ushauri hutolewa kwa baadhi ya waombaji kupanga tarehe nyingine muafaka.

## *Ukaaji Ndani ya Bunge*

Kanuni ya 140 ya Kanuni za kudumu za Bunge inaelekeza kuwa, Spika ataweka utaratibu maalumu wa Ukaaji wa Wabunge ndani ya Bunge bila kuathiri mpangilio ufuatao:

- Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni (Waziri Mkuu) anakaa kiti cha kwanza akifuatiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mawaziri upande wa kulia wa Spika.
- Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni anakaa kiti cha kwanza akifuatiwa na Wasemaji Wakuu wa Kambi ya Upinzani, upande wa kushoto wa Spika.
- Endapo hakuna Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani aliyechaguliwa na chama chenye haki ya kuchagua Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni lakini Wabunge wa upinzani wapo, basi Wabunge hao watakaa upande wa kushoto wa Spika.

## *Mambo ya Kuzingatiwa*

Vikao vya Mikutano ya Bunge huanza saa 3.00 asubuhi na kwa kawaida huendelea hadi saa 7.00 mchana ambapo husitishwa. Wabunge hurejea tena saa 10.00 jioni na Kikao huendelea hadi saa 2:00 usiku ambapo Bunge huairishwa mpaka siku inayofuata. Hivyo basi, wageni wote wanapaswa wawe wameketi katika maeneo husika kabla ya saa 2:45 asubuhi na saa 09:45 jioni kabla ya vikao kuanza.

Kwa kuzingatia Kanuni za Kudumu za Bunge, wageni wote wanapaswa kuvaa mavazi ya heshima. Baada ya kufika katika milango ya kuingilia, wageni wote husajiliwa na kupatiwa vitambulisho maalumu vitakavyovaliwa wakati wote wawapo katika maeneo ya Bunge.

Ndani ya Ukumbi wa Mikutano ya Bunge, wageni wanapaswa kufuata na kuzingatia masharti yafuatayo:

- Kukaa kimya na kwa heshima inayostahili hadi watakapotoka nje ya Ukumbi huo
- Kuingia na kutoka Ukumbini kwa staha
- Hairuhusiwi kusoma kitabu chochote, gazeti, barua au hati nyingineyo ambayo si orodha ya shughuli za Bunge
- Hairuhusiwi kuandika wala kurekodi jambo lolote linalozungumzwa, isipokuwa tu kama ni wawakilishi wa vyombo vya habari au maafisa wa serikali.
- Hairuhusiwi kuvuta sigara au kiko wakati wowote wakiwa ndani ya Ukumbi wa Mikutano ya Bunge au mahali popote nje ya Ukumbi huo ambapo kuna mahali pa kukaa wageni
- Kuzima simu za mikononi
- Hairuhusiwi kuingia na kamera wala kupiga picha kwa kutumia kifaa chochote kile
- Hairuhusiwi kufanya jambo au kitendo chochote ambacho kinaweza kuvuruga amani na utulivu Bungeni
- Kurejesha kitambulisho wakati wa kuondoka maeneo ya Bunge

Taratibu hizi zimewekwa ili kulinda utulivu na amani katika maeneo ya Bunge. Mara baada ya kushuhudia vikao vya Bunge vinavyoendeshwa, wageni wanaotembelea Bunge hupata fursa ya kupewa Elimu juu ya Historia ya Bunge, Muundo na Majukumu ya Bunge, Nafasi ya Upinzani Bungeni ikiwa ni pamoja na kutembelea maeneo mbali mbali katika Viwanja vya Bunge kujionea mandhari ilivyo.

"Kumbuka ni haki ya kila mtu kutembelea Bunge ili kujionea Shughuli za Uwakilishi zinavyotekelezwa. Itumie fursa hii kutembelea Bunge lako"

*******




*Wanafunzi na Wageni Mbalimbali wanaotembelea Bunge kwa ajili ya Mafunzo hupata fursa ya kupatiwa*



*Elimu kuhusu kazi za Bunge na kutembezwa katika Viwanjwa vya Bunge*



*Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashillilah akizungumza na wanafunzi waliotembelea Bunge*

**Kimetayarishwa na**

**Ofisi ya Bunge**
**Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano**
**S.L.P. 9133**
Simu: +255 22 2118505,
Nukushi: +255 22 2112538,

Ofisi ya Bunge, S.L.P. 941
2 Barabara ya Bunge
41490 Dodoma
Simu: +255 26 2322761-5,
Nukushi: +255 26 2324218
Barua pepe: info@bunge.go.tz
Tovuti: www.parliament.go.tz

**Supported by:**

***Legislatures Support Project (LSP)***